

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULIZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA TISA

02 MEI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA TISA – TAREHE 02 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAJI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA MAJI:

Taarifa ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

154. MHESHIMIWA SELEMANI SAID BUNGARA (KILWA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Kilwa haina Jokofu la kuhifadhi maiti na pia majengo yake mengi ni chakavu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua Jokofu jipya sambamba na kukarabati majengo ya Hospitali hiyo.

155. MHESHIMIWA YOSEPHER FERDINAND KOMBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kuna uhaba wa Watumishi na vitendea kazi katika Idara ya

Ardhi na Maliasili – Wilaya ya Muheza kunakosababisha kuazima Watumishi na vifaa kutoka Halmashauri nyingine:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaajiri Watumishi na kununua vitendea kazi katika Idara hiyo;
- (b) Je, Serikali iko tayari kuwawekea Wananchi Wanasheria ili kusaidia kutatua migogoro ya ardhi.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

156. MHESHIMIWA DKT. RASHID MOHAMED CHUACHUA (MASASI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Jeshi la Polisi limekuwa likifanya kazi katika mazingira magumu sana kutokana na uchakavu wa vitendea kazi pamoja na kukosekana kwa magari ya kutosha:-

- (a) Je, ni lini Serikali itawapatia magari Askari Polisi wa Wilaya ya Masasi kutokana na kutokuwa na magari ya kutosha;
- (b) Je, ni lini Serikali itarekebisha utaratibu uliopo ambapo Askari wanalazimika kutoa pesa zao za mfukoni kuwapa chakula Mahabusu;

(c) Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za Askari katika Wilaya ya Masasi.

157. MHESHIMIWA ISSA ALI MANGUNGU (MBAGALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Serikali ilianzisha Kanda Maalum ya Kipolisi Dar es Salaam na kufanya Wilaya ya Temeke kuwa Mkoa wa Kipolisi; tangu Temeke iwe Mkoa wa Kipolisi kumekuwa na ongezeko kubwa la uhalifu hasa maeneo ya Jimbo la Mbagala:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo cha Mkuu wa Polisi Wilaya ya Mbagala;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Vituo vya Polisi na kuviongezea Askari, vitendea kazi na kujenga nyumba za Askari katika maeneo ya Jimbo la Mbagala.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**DODOMA
02 MEI, 2019**



**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**

